



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE



Simu Na: +255 (026) 2740016
Nukushi: +255 026 2740103
BaruaPepe: ded@makete.go.tz
Tovuti: <http://www.maketedc.go.tz>
Unapojibu tafadhali taja;
Kumb. Na. EA.172/302/01/170

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri Wilaya ya Makete,
4 Barabara ya Bomani,
59582 MAKETE, NJOMBE,
S.L.P 6, MAKETE
08 Julai, 2024

TANGAZO LA KAZI

Kwa mujibu wa Kibali cha Ajira mpya chenye Kumba Na. FA.97/228/01/09 cha tarehe 25/06/2024 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia Watanzania wote wenye sifa za kuomba nafasi ya kazi kama ifutavyo:-

1. DEREVA II-NAFASI 7

1.1 Sifa za Mwombaji

- Awe mwenye elimu ya kidato cha nne au sita
- Awe na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajari.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

1.2 MAJUKUMU

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa Gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya Gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa Gari.

1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za Mshahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B1 kwa mwezi.**

1.4 MASHARTI YA WAOMBAJI WOTE

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Waombaji lazima waambatanishe nakala za vyeti vifuatavyo:-
 - a. Cheti cha Taaluma
 - b. Cheti cha mtihani wa kidato cha nne au sita
 - c. Cheti cha kuzaliwa
 - d. Nakala ya kitambulisho cha NIDA
 - e. Picha mbili za Passport size za hivi karibuni.
 - v. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo ya kidato cha nne au sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**) HAVITAKUBALIWA.
- vi. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- viii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **29, Julai, 2024** saa 9:30 Alasiri. Baada ya tarehe hiyo kupita maombi hayatapokelewa, na watakao chaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.maketedc.go.tz na kwenye mbao za matangazo za Halmashauri.

2. Muhimu, kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zile zinazihitajika. Barua ya maombi itumwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P. 6,
MAKETE.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Makete www.maketedc.go.tz

Limetolewa na:



William M. Makufwe
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya

MAKETE.

Nakala: Mbao za Matangazo
Halmashauri ya Wilaya
MAKETE.

MKURUGENZI MTENDAJI KW.
MAKETE